

Jina: .....

Nambari: .....

Darasa: .....

Sahihi .....

Tarehe: .....

**102/3**

**KISWAHILI  
KARATASI YA 3  
FASIH**

**MUDA: 2 1/2**

**MUHULA WA TATU 2019**  
*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya (K.C.S.E)*  
**KIDATO CHA NNE**

**Kiswahili  
Fasihi**

**MAAGIZO**

- Jibu maswali manne pekee. Swali la kwanza ni la lazima
- Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu zilizobaki
- Usijibu maswali **MAWILI** kutoka sehemu moja.

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

<b>SWALI</b>	<b>UPEO</b>	<b>ALAMA</b>
1	20	
2	20	
3	20	
4	20	
<b>JUMLA</b>	<b>80</b>	

**SWALI LA LAZIMA**

**1.HADITHI FUPI** **ALAMA 20**

**TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE :Alifa Chokocho Na Dumu Kayanda  
Mtihani wa Maisha**

1. “..Acha nijiondokee duniani niwaacie wafanisi wafanikie.”
  - a) Eleza muktadha wa dondo hili. Alama 4
  - b) Taja na ufanue sifa tatu za msemaji. Alama 6
  - c) Eleza jinsi maisha ya msemaji yanavyoafiki anwani ya hadithi. Alama 10

**2.RIWAYA                    CHOZI LA HERI : Assumpta Matei                    ALAMA 20**

2. Eleza jinsi **maudhui ya ufisadi** yalivyoshughulikiwa katika riwaya ya Chozi la Heri. Alama 20
3. “...*liandikwalo ndilo liwalo? Since when has man ever changed his destiny?*”
- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. Alama 4
  - b) Bainisha mbinu tatu za kimitindo zinazojitokeza katika dondoo hili. Alama 6
  - c) Kwa kuzingatia hoja **kumi**, jadili jinsi ambavyo hali ya, “ **liandikwalo ndilo liwalo**”, inavyojitokeza katika Chozi la Heri. Alama 10.

**3.TAMTHILIA                    KIGOGO : Pauline Kea                    ALAMA 20**

4. “Utarwala wa Majoka katika jimbo la Sagamoyo umejaa sumu ya nyoka.” Jadili. Alama 20
5. Eleza jinsi mbinu zifuatazo ziliviyotumika katika tamthilia ya Kigogo
- i) Kinaya Alama 6
  - ii) Majazi Alama 8
  - iii) Jazanda Alama 6

**4.FASIHI SIMULIZI                    ALAMA 20**

6. a) Eleza **aina** tano za wahusika wa fasihi simulizi. Alama 10
- b) Eleza sifa za wahusika wa mighani. Alama 10
7. a) Eleza namna amabavyo hadhira wanahusishwa katika utambaji. Toa hoja nne. Alama 8
- b) Taja na ueleze sifa nne bainifu za hadithi. Alama 4
- c) Taja viungo vinavyopambanua muundo wa nyimbo katika jamii Alama 4
- d) Andika majukumu manne ya nyimbo katika jamii Alama 4

**5.USHAIRI                    ALAMA 20**

**8. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Zitavuma,  
Zitakoma,  
Nitakwima,  
Mti-mle.

Na muda nikisimama,  
Nitatonga nudhuma,  
Kwa tenzi zilizo njema,  
Nilisifu mti – mle.

Tazipanga tathlitha, tungo zilizo na hekima,  
Za huba na thiatha, za kuburudi mitima,  
Mashairi mabuthutha, musome mnaosoma.

Mti nishainukia, namea kuwa mzima,  
Mizizi yadidimia, ardhini imeuma,  
Nanena kitarbia, tungo zilizo adhama  
Japo ni tungo za zama, mti-mle hutumia.

Zingavuma zitapusa, pepo kali zitakoma,  
Dharuba kinitikisa, mti-mle huinama,

Huyumba nikaziasa, matawi yakakingama,  
Gharika ikishapisa, hurudi nikawa wima,  
Na tongo za takhimisa, mti-mle huzipima.

### Maswali

- (a) Shairi hili ni la kimapokeo. Toa sababu mbili **kuunga** kauli hii. (Alama.2)
- (b) Taja **bahari kuu** ya ushairi ambayo imetumiwa na mshairi. **Fafanua.** (Alama.2)
- (c) Fafanua dhamira ya mshairi. (Alama.2)
- (d) Kwa kutoa mifano bainisha tamathali mbili za usemi zilizotumika katika shairi hili. (Alama.2)
- (e) Eleza jinsi mshairi ametumia idhini ya ushairi katika utungo huu. (Alama.2)
- (f) Andika ubeti wa nne kwa lugha natharia. (Alama.4)
- (g) Mshairi anamaanisha nini anaposema zingavuma zitapusa, pepo kali zitakoma, ‘ (Alama.2)
- (h) Eleza toni ya shairi hili. (Alama.2)
- (i) Eleza maana ya msamiati ufuataao.
  - i) Nitatongoa (Alama.2)
  - ii) Zitapusa.